

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI
SHULE YA SEKONDARI MILOLA
S.L.B 355 - MILOLA LINDI

MZAZI/MLEZI WA:

S.L.B 1070

MILOLA

LINDI

Ndugu,

YAH: KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

Napenda kukujulisha kuwa mwanao ni miongoni mwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga katika shule ya sekondari Milola kidato cha kwanza 2021.

Shule yetu itafunguliwa siku ya Juma tatu tarehe 11/01/2021 na mwanao anatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa

Mwanao anatakiwa awe na vitu vifuatavyo:

1. SARE ZA SHULE:

A. WASICHANA:

- ❖ Blauzi mbili (2) nyeupe mikono mirefu isiyobana
- ❖ Sketi mbili ndefu za kijani
- ❖ Shungi (hijabu) nyeupe pana na kubwa inayofika mpaka kifuni
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2) vyenye visigino vifupi
- ❖ Soksi nyeupe Jozi mbili (2)

B. WAVULANA

- ❖ Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mifupi
- ❖ Suruali Jozi mbili (2) rangi ya kaki
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2) vyenye visigino vifupi
- ❖ Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- ❖ Mkanda mweusi wa ngozi

2. TAALUMA:

- ❖ Madaftari makubwa kumi na mbili (12)
- ❖ Kamusi ya kingereza kwa Kiswahili
- ❖ Mkebe (Mathematical set)
- ❖ Kalamu za wino na risasi
- ❖ Ruled paper (rim) kwa ajili ya mazoezi na mitihani (muhimu saana afike nayo siku ya kuripoti bila kukosa)

3. MICHEZO:

- ❖ Tisheti rangi ya bluu kwa wote
- ❖ Bukta (wavulana) track (wasichana)
- ❖ Raba za michezo na soksi za michezo

4. USAFI NA MAZINGIRA

- ❖ Fagio na jembe kubwa

Pamoja na maelezo hayo napenda kukufahamisha kuwa shule yetu ni ya serikali hivyo inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kisheria.

Hivi vyote vinalenga kumjenga na kumlea kijana wako katika misingi ya maadili, nidhamu na makuzi mema. Anatakiwa atii na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule akiwa ndani na nje katika kipindi chake cha uanafunzi.

Kijana wako atatakiwa kuwepo shule na kuhudhuria mafunzo katika muda wote wa uanafunzi wake.

Aidha ni marufuku kwa mwanao kwenda au kuonekana sehemu kama kumbi za starehe, vilabu vya pombe, vigodoro, na kuwa na matumizi ya lugha chafu.

Fauka na hayo makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kijana wako kufukuzwa shule (kusitishwa masomo)

1. Wizi wa aina yoyote
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji na ulawiti
4. Kupiga au kupigana
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya uma
6. Kudharau bendera
7. Ulevi wa aina yoyote
8. Kuo au kuolewa, kupata mimba au kusababisha mimba, kutoa mimba au kusaidia kutoa mimba
9. Kuvuruga amani, kushiriki au kusababisha mgomo
10. Utoro
11. Kumiliki au kutumia simu

MUHIMU

Kila mzazi au mlezi hanabudi kuzisoma na kuzizingatia sheria, kanuni na taratibu hizi kwa makini na kushauriana na kijana wako katika utekelezaji.

Fomu hii utakuja nayo siku ya kumleta kijana wako.

Nakutakia maandalizi mema:

.....

Mwalimu MANYANYA M

0622 317 671 au 0782 317 671

HATI YA MAKUBALIANO:

Mimi:..... (mwanafunzi) nimesoma fomu hii kwa makini na kuelewa. Naahidi nitatekeleza sheria kanuni na taratibu za shule kama zilivyoainishwa. Nitawaheshimu walimu, wazazi/walezi wakubwa na wadogo pamoja na wanajamii wanaonizunguka nikiwa ndani na nje ya shule. Sitokuwa mtoro au kuacha shule kwa sababu yoyote labda kitokee kifo

Jina la mwanafunzi:.....saini.....tarehe.....

Mimi:.....(mzazi/mlezi) wa mtajwa hapo juu nimesoma na kuelewa fomu hii. Naahidi kutekeleza majukumu yangu pia nitatoa ushirikiano kwa walimu katika kuhakikisha kijana wangu anakua na mahudhurio mazuri shuleni, kusoma kwa bidii na matokeo mazuri darasani

Jina la mzazi/mlezi:..... saini:..... tarehe:.....